# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KWA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa heshima na taadhima natanguliza shukrani zangu za dhati kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na utukufu kwa kutujaalia sote kuwa na afya njema na kutuwezesha kufika hapa leo kuendelea na shughuli za ujenzi wa taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inachukuwa fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake makini ambao una nia ya kuleta mapinduzi kwa sekta ya kilimo na mifugo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu pia inatoa pongezi zake za dhati kwa Makamo wa kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdallah, kwa kumshauri vyema Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake mazito ya kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Pamoja na timu yake inayoongozwa na Katibu Mkuu, ndugu Seif Shaaban Mwinyi kwa kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya taifa letu. Aidha Kamati inamshukuru kwa dhati Katibu Mkuu aliyepita ndugu Maryam

Juma Sadalla kwa kusimamia vyema majukumu ya Wizara hii kwa kipindi chote cha uongozi wake. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amsimamie vyema katika utekelezaji wa majukumu yake katika taasisi aliyohamishiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Hata hivyo kwa namna ya pekee naomba niwapongeze wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu yao ya msingi katika kuipatia Wizara hii miongozo na ushauri unaofaa katika kufikia malengo yaliyokusudiwa. Naomba niwatambue wajumbe hao kama ifuatavyo:

1. Mheshimiwa Yussuf Hassan Idd — Mwenyekiti
2. Mheshimiwa Aza Januar Joseph — M/Mwenyek
3. Mheshimiwa Mwanajuma Kassim Makame — Mjumbe
4. Mheshimiwa Nassor Salim Ali — Mjumbe
5. Mheshimiwa Saada Ramadhan Mwedwa — Mjumbe
6. Mheshimiwa Said Saleh Salim — Mjumbe.
7. Ndg. Mwaka Mwinyi Waziri — Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Jumla ya maagizo 77 yalitolewa na Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii katika kikao cha Februari 2022 kwa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Malisili na Mifugo. Kati ya maoni hayo 13 yalihusu Idara ya Umwagiliaji maji kwa mabonde ya Saninga, Cheju na Kilombero. Maoni 18 yalihusu Idara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula, Maoni 13 yameelekezwa kwa Wakala wa Serikali na Huduma za Matrekta, Maoni 10 yameelekezwa katika Idara ya Maendeleo ya Mifugo, Maoni 16 yameelekezwa katika Idara ya Misitu na maoni 7 katika taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kiujumla, Kamati imeridhika na utekelezaji wa maagizo hayo, hata hivyo Kamati haikusita kutilia mkazo juu ya utekelezaji wa baadhi ya maagizo kwa lengo la kuboresha ufanisi katika utendaji kazi katika taasisi zetu kama ifuatavyo:

## UHARIBIFU WA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI

**Mheshimiwa Spika,**

Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji maji ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo. Mradi huu ulihusisha ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhia maji ya kumwagilia, ujenzi wa misingi ya kumwagilia na kutolea maji ya ziada, ujenzi wa ploti na ujenzi wa barabara za shambani kwa kiwango cha kifusi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kufuatia kadhia kubwa ya uharibifu wa miundombinu ya Umwagiliaji ambayo imetumia gharama kubwa katika matengenezo yake, Kamati iliishauri Wizara ya Kilimo kufanya hima kushirikiana na Kamati za Ulinzi za Mikoa, Wilaya na Shehia ili kukabiliana na tatizo la uharibifu wa miundombiunu ya Umwagiliaji ambayo kamati iliibani wakati wa ziara katika mabonde hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na umuhimu wa miundombinu hii ya Umwagiliaji kwa wakulima katika mabonde yote yaliyopitiwa na mradi huu, Kamati inaendelea kutoa ushauri wake kwa Wizara, kushirikiana na Idara ya Kilimo kutoa elimu ya kutosha kwa jamii juu ya kuitunza, kuihifadhi na kuilinda miundombinu hiyo, Uwepo wa miundombinu hii ni hatua moja kubwa ya maendeleo katika sekta ya kilimo nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati inachukuwa nafasi hii kuipongeza sana Serikali pamoja na Wizara ya Kilimo,Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa kukabidhi baadhi ya mabonde haya kwa wakulima. Siku ya tarehe 02 Agosti mwaka huu, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, ilikabdhi bonde la Umwagiliaji la Kinyasini kwa wananchi baada ya kukamilika kwake, ambapo wakulima 1200 tayari wameshakabidhiwa mashamba kwa ajili ya kuanza matayarisho ya kilimo kwa msimu huu. Kufunguliwa kwa bonde hili kunaweza kufungua fursa kwa wakulima kuongeza uzalishaji zaidi na kuweza kujikimu kimaisha.

## USHIRIKISHWAJI WA JAMII KATIKA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati iliiagiza Wizara kuishirikisha jamii kikamilifu wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kupunguza migogoro baina ya wananchi na Serikali wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Ni dhahiri kwamba, miradi ya maendeleo inahusisha jamii moja kwa moja kwa kutoa maeneo yao na kuharibika kwa vipando vyao, kwa ajili ya kupisha miradi iendelee, hivyo ushirikishwaji mdogo wa jamii wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyomo ndani ya Wizara, inapelekea kuibuka kwa changamoto kadhaa ambazo zinaweza kuchangia katika kuzorotesha utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Endapo Wizara itawashirikisha wanajamii kikamilifu katika hatua zote za utekelezaji wa miradi, Wizara itaweza kutatua baadhi ya changamoto katika ngazi ya chini kabisa ikiwa ni pamoja na kuwapa nafasi wanajamii kutoa maoni na ushauri ulio sahihi na hatimae kuiwezesha miradi hii kukamilika na kuleta tija iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inayasema haya kutokana na ukweli kwamba, bonde la umwagiliaji Chaani lilishindwa kutumika kwa wakati baada ya kukamilika ujenzi wa miundombinu yake, sababu ni ushirikishwaji mdogo wa wanajamii kijijini hapo. Hali iliyopelekea kurudisha nyuma juhudi za serikali za kuwaletea maendeleo wananchi wake.

## UPUNGUFU WA MABIBI NA MABWANA SHAMBA

**Mheshimiwa Spika,**

Uhaba wa watendaji hawa katika sekta ya kilimo ni changamoto kubwa inayoathiri matokeo mazuri kwa wakulima nchini. Kamati imebaini kwamba utekelezaji wa agizo la kuongeza idadi ya mabibi na mabwana shamba nchini kwa wizara ya Kilimo bado haujatekelezeka ipasavyo, kutokana na ukweli kwamba, wakulima waliowengi hawafikiwi kwa wakati, jambo linalowakosesha fursa ya kupatiwa huduma ya ushauri kuhusu uzalishaji bora wa mazao yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliji, Maliasili na Mifugo kushirikiana na Wizara ya Katiba, Sheria ,Utumishi na Utawala Bora kuharakisha zoezi la uajiri wa watendaji hawa kwa maslahi mapana ya wakulima na wananchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati inashauri, ni vyema mabibi na mabwana shamba waliopo wawe tayari kujitolea katika kuhakikisha wanawafikia wakulima kwa wakati kwa lengo la kuwapatia ushauri kuhusu kilimo chao na hatimae waweze kuzalisha mazao yaliyo bora. Aidha, Mabibi na mabwana shamba hawana budi kufanya tafiti katika mazao ya wakulima, ili kusudi waweze kupambana na wadudu ambao huharibu mazao hayo.

ULINZI NA UHIFADHI WA RASILIAMLI MISITU

**Mheshimiwa Spika,**

Misitu ni rasilimali muhimu ambayo endapo itahifadhiwa vyema, inaweza kutoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya taifa letu. Kamati ilitoa ushauri kwa Wizara ya Kilimo kutoa elimu kwa jamii juu ya kuilinda na kuihifadhi misitu iliyomo ndani ya hifadhi zetu nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Ni wazi kabisa, hujuma mbalimbali zinaendelea kufanywa na wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya hifadhi za misitu kwa kukata kuni, kuchoma moto na kuvuna asali, hali inayoathiri viumbe hai vilivyomo ndani ya misitu hiyo ambavyo ni vivutio vikubwa kwa wageni wanaofika katika misitu hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Taifa limeutambua tangu uhuru hadi hivi sasa, umuhimu wa misitu na wanyamapori waliomo ndani yake, ambao unaozidi kuongezeka siyo tu katika kuwavutia watalii wengi hapa nchini, lakini pia katika kutunza mazingira. Mazingira hayo ni yale yanayotuzunguka yanayojumuisha hewa, udongo na maji ili nchi yetu iweze kutoa mchango wake stahiki katika kupunguza kasi ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yameikumba dunia. Aidha, uchumi wa Tanzania unategemea kwa kiasi kikubwa misitu

iliyopo, ambapo ni urithi mwema kwa vizazi viliopo na vijavyo, hivyo kuwepo kwake hutegemea zaidi uhifadhi wake na matumizi endelevu katika jamii inayotuzunguka.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mnasaba huu, Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Kilimo, kuendelea kushirikiana na jumuiya mbalimbali zilizoundwa kwa lengo la kuilinda na kuihifadhi misitu hii kwa mustakabali mwema wa taifa letu. Kamati inaamini kwamba, kuimarika kwa ulinzi na uhifadhi wa misitu hii kutasaidia sana katika kuongeza pato la taifa, kutatoa fursa kwa wageni kufika na kujionea uasili na maajabu yaliyomo katika misitu hii.

## MTAMBO WA KUHIFADHIA GESI YA KUPANDISHIA NG'OMBE WA SINDANO

**Mheshimiwa Spika,**

Moja kati ya maagizo yaliyotolewa na Kamati kwa Idara ya Maendeleo ya Mifugo ni kununua mtambo mwengine mpya wa kuhifadhia gesi ya kupandishia ng'ombe wa sindano na kuacha kuufanyia matengenezo mtambo uliopo kutokana na uchakavu wake, kuendelea kuufanyia matengenezo mtambo huo ni kuitia hasara Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuitengea fedha Idara hii kwa lengo la kununua mtambo huu utakaogharimu jumla ya shilingi za kitanzania **Milioni 650**. Kutokana na umuhimu wa mtambo huu, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Maendeleo ya Mifugo kuandaa na kuharakisha mpango kazi wake wa manunuzi ya mtambo huu ndani ya mwaka huu wa fedha, lengo ni kuwasaidia wafugaji wetu waweze kuzalisha zaidi.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na hali hii, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuandaa mazingira bora ya kuuweka mtambo mpya utakaonunuliwa hasa tukizingatia mazingira yaliyopo hivi sasa sio rafiki.

## HITIMISHO

Mwisho kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi **Mheshimiwa Spika,** kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati, pamoja na kuwashukuru wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kumega wakati wao na kunisikiliza kwa makini wakati nikiwasilisha hutuba hii. Sasa wakati umefika niwaombe wajumbe wa Baraza lako waijadili na kuichangia hotuba hii kwa mustakbali wa taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Mimi binafsi na kwa niaba ya Kamati ninayoiongoza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha.

**Ahsante,**

………………………………

Mhe.Yussuf Hassan Idd.<br>
Mwenyekiti,<br>
Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii<br>
Baraza la Wawakilishi<br>
**Zanzibar.**